



DSPACE

<https://dspace.org/>

Si tendi zote za kabla ya karne ya ishirini ni utambaji wa kingano nyengine ni ufunzaji: Kiyelelezo cha utendi wa siri li asrari

Karama, Mohamed; Chimerah, Rocha; Mutiso, Kineene

2021

Jarida la Afrika mashariki la masomo ya Kiswahili

: <https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.349>

Karama, M., Chimerah, R., & Mutiso, K. (2021). Si Tendi zote za Kabla ya Karne ya Ishirini ni Utambaji wa Kingano Nyengine ni Ufunzaji: Kiyelelezo cha Utendi wa Siri li Asrari. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 3(1), 51-57.



East African Journal of Swahili Studies

eajss.eanso.org

Volume 3, Issue 1, 2021

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>



EAST AFRICAN
NATURE &
SCIENCE
ORGANIZATION

Original Article

Si Tendi zote za Kabla ya Karne ya Ishirini ni Utambaji wa Kingano Nyengine ni Ufunzaji: Kiyelelezo cha Utendi wa Siri li Asrari

Mohamed Karama¹, Rocha Chimera² & Kineene wa Mutiso³

¹Chuo Kikuu cha Kabianga, S.L.P 2030 – 20200, Nairobi, Kenya.

* ORCID ID: <https://orcid.org/0000-0003-2341-9966>; Barua pepe ya mawasiliano: mkarama@kabianga.ac.ke

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.349>

Tarehe ya Uchapishaji: IKISIRI

26 Juni 2021 Fikra iliyomo katika mawanda ya fasihi ya Kiswahili ni kuwa utendi ni maelezo marefu ya mapisi ya jamii kiushairi. Makala haya yanaoka kuonesha kwamba si tendi zote zenye madhumuni haya. Kupitiya Utendi wa Siri li Asrari tunaonesha kwamba mthunzi Mwanalemba alikuwa na niya tangu mwanzo ya kuweka darasa kuhusu hirizi ya majina ya Mwenyezi Mungu. Darasa hii ameigawanya kama namna taasisi za kielimu zinavopendekeza ienreshwe kiskuli na ameyatowa mawazo yake kitaalamu. Nadhariya ya Usemizano kupitiya dhana ya Unrimi imetusaidiye kuuwangaziya utendi huu na tumefaidika na vigezo va: maudhui, uteuzi wa misamiati na mitinro ya uwasilishaji, na muktadha wa matumizi ya maneno hayo kama njiya ya kutambuwa aina ya lugha inayotumika. Kwa kwangaziya mitinro ya uwasilishaji katika darasa ya hirizi tumepata kujuwa kwamba mthunzi alikuwa na dhamira ya kutufunza badala ya kutamba hadithi ya kingano.

APA CITATION

Karama, M., Chimera, R. & Kineene, M. (2021). Si Tendi zote za Kabla ya Karne ya Ishirini ni Utambaji wa Kingano Nyengine ni Ufunzaji: Kiyelelezo cha Utendi wa Siri li Asrari. *East African Journal of Swahili Studies*, 3(1), 51-57. <https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.349>.

CHICAGO CITATION

Karama, Mohamed, Rocha Chimera and Mutiso Kineene. 2021. "Si Tendi zote za Kabla ya Karne ya Ishirini ni Utambaji wa Kingano Nyengine ni Ufunzaji: Kiyelelezo cha Utendi wa Siri li Asrari". *East African Journal of Swahili Studies* 3 (1), 51-57. <https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.349>.

HARVARD CITATION

Karama, M., Chimera, R. and Kineene, M. (2021) "Si Tendi zote za Kabla ya Karne ya Ishirini ni Utambaji wa Kingano Nyengine ni Ufunzaji: Kiyelelezo cha Utendi wa Siri li Asrari", *East African Journal of Swahili Studies*, 3(1), pp. 51-57. doi: 10.37284/eajss.3.1.349.

IEEE CITATION

M. Karama., Chimera, R. and Kineene, M., "Si Tendi zote za Kabla ya Karne ya Ishirini ni Utambaji wa Kingano Nyengine ni Ufunzaji: Kiyelelezo cha Utendi wa Siri li Asrari", *EJSS*, vol. 3, no. 1, pp. 51-57, June. 2021.

MLA CITATION

Karama, Mohamed, Rocha Chimera and Mutiso Kineene. "Si Tendi zote za Kabla ya Karne ya Ishirini ni Utambaji wa Kingano Nyengine ni Ufunzaji: Kiyelelezo cha Utendi wa Siri li Asrari". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 3, no. 1, June. 2021, pp. 51-57 doi:10.37284/eajss.3.1.349.

UTANGULIZI

Utendi wa Siri li Asrari (soma Siri) una beji tisaini na zaidi zenye kuzungumziya hirizi ni nini na umuhimu wake katika maisha haya na ya akhera. Mwanamwarabu binti Bwanalemba¹ (ajulikana piya kama Mwanalemba), mthunzi mwanamke wa utendi huu, anamsemesha mhusika wake, Malaika Jibril, katika beji hizo kwa njia isiyo ya kimasimulizi ya kingano yenye kueleza 'hadithi' au 'hekaya' ili wasikilizaji wasikize na kufurahiya yanayot'ongolewa. Makala haya yaonesha kwamba Siri ni darasa yenye muunro maalumu wa kiuwasilishaji wa kitaalamu na una malengo makhsusi yanayotarajiwa kupatikana. Imetuthubutukiya katika mapitiyo yetu kuhusu utendi huu kuwa suala hili la Siri ina shabaha ya kufunza halijashughulikiwa kamwe.

Vijelezi vinavyotolewa na fikira inayoenrelezwa kuhusu utendi ni kwamba, "ni ut'ungo mrefu wenye kwelezeya kisa au jambo kuhusu mtu/jamii" (Shariff, 1988:94). Tendi maarufu katika fasihi ya Kiswahili *Hamziya*, *Al Inkishafi*, *Mwanakupona*, *Rasil Ghuli*, *Mwana Fatuma* zaeleza kuhusu mathukio fulani katika maisha ya mthu (aghalabu Mthume Muhammad) na majagina wa Kiislamu. Utendi wa *Mwanakupona* umejitowa katika kunri hili la visa na kujiangaza kama mawaidha (wasiya). Ijapokuwa Siri ni masimulizi ya vita baina ya Mthume Muhammad (nguli wa utendi huu) na Andharuni (nruli wa utendi huu), sehemu hii ya vita, ambayo iko mwanzo wa utendi wenyewe, ina lengo la kitaalamu na wala si kutamba kisa au hadithi kama tutakavothibitisha katika makala haya.

Mapitiyo yetu ya yaliyoandikwa kuhusu utendi huu yaonesha kwamba bado hayajashughulikiya mada hii ya lengo la kiufunzaji – kwa maana ya kufanya darasa kuhusu jambo kwa mpangiliyo wa kitaalamu au kiskuli. Maelezo kuhusu istilahi ya tendi katika fasihi ya Kiswahili inajulikana, na kushikiliwa nriwo

haswa mfano Parker (1982) akinukuliwa na Shariff (1984, uk. 152), kuwa ni maudhui yenye kueleza kisa kingano. Anapozungumziya uwamilifu wa utendi Shariff (1991, uk. 45) anasema kwamba, "utendi una umuhimu mkubwa katika kuelimisha na kufurahisha jamii." Makala haya yaonesha kwamba kwelimisha huku kwatokana na kufunza kwenye mandhari ya darasani. Njogu na Chimera (1999) na Chimera (1989) wanaotowa kiyelelezo cha namna darasa latakikana liyenreshwe wakaŋi wa ufunzaji kama inavyopendekezwa na Taasisi ya Kutayarisha Mtalaa wa Elimu ya Kenya (K.I.C.D) na kiyelelezo hichi nriho kinachotufahamisha kwamba kwelimisha kuna mfumo na mfumo huu una miyunro inayotumiwa ili lengo linalotarajiwa lipatikane. Makala haya hayaotofwata, mguu kwa mguu, mpangiliyo huu wa Taasisi; imetoshleza kutuza kwamba kuna miyunro ya kufunza na mthunzi aliitumiya miyunro fulani ili kufunza hadhira yake – wasomaji na wasikilizaji wa utendi wake.

Bakhtin (1986) anasema kwamba lugha ina lugha nyingi nrani yake ambazo hujitokeza katika mawanda tafauti tafauti na miktadha tafauti tafauti. Lugha hii inabeba maudhui ya yatakayosemwa; mitinro ya lugha makhsusi itakayotumiwa kuyasema mawazo hayo; na, muhimu zaidi, muktadha upi utakaosababisha mawazo hayo kusemwa kwa namna inavyotarajiwa. Mambo haya matatu nriyo yanayoleta athari ya kuyasema maneno hayo. Kutokana na msingi wa nadharia hii ya Usemezano inayoshadidia kuwako kwa nrimi katika lugha moja basi makala haya yatashika aina moja ya nrimi zilizoratibishwa nayo ni: usemaji wa kitaalamu. Bakhtin (1986) anasema kila ulimi (lugha) una misamiati na mitinro tafauti wa uwasilishaji inayoitambulisha kuwa ni sajili kamili tafauti na sajili nyengine. Kwa mntarafu hii ya tafauti za kimitinro, makala haya yaangazia namna lugha hii ya kitaalamu inavojitokeza na

¹Katika Dammann (1940:274) "bwanalemba" inatanbihishwa kuwa ni lakabu. Kulingana na Ustadh Muhammad Al Beidh (r.a) katika "Hali ya Afrika Mashariki" ZCTV Live Agosti 2011 kwenye Youtube,

alimtaja Bwanalemba kuwa Ahmad bin Alwy bin Muhammad Faqihil Muqaddam "Swahibu A'maim" (mwenye malemba).

kuuṭafautisha Siri na ṭendi nyengine maarufu kiufunzaji.

UFUPISHO WA SIRI

Siri unaanza kwa kuṭhongolewa hadithi ya vita baina ya Mṭhume Muhammad na Andharuni. Andharuni aliwanyanya wakaaji wa mji wa kwao na wanaṭi wakamlalamikiya Mṭhume Muhammad kuwaokowa na viṭimbi va Andharuni. Mṭhume Muhammad akaitikiya mwitḥo huwo kwa kupeleka jeshi la waislamu kuonrosha udhalimu wa Andharuni. Awali, Andharuni alionesha ujabari mkuu kwa kuwapiga waislamu bila huruma kuṭokana na nguvu za hirizi aliyoirithi kuṭoka kwa mababu zake. Mṭhume Muhammad kusikiya hayo alikuja kuviyona vita hivi na akaomba nusura kwa Mola ili waislamu madhaifu wasiangamizwe na Andharuni. Mungu akamjulisha, kupitiya malaika Jibril, Mṭhume Muhammad kwamba Andharuni ana hirizi na nriyo inayompa nguvu hizo za kiajabu. Mṭhume Muhammad akaomba apawe yeye hirizi hiyo na alipopawa bado alienreleya kushinrwa katika vita hivi. Baadaye, Mṭhume Muhammad akaomba ṭena kwa Mungu na akamshinra Andharuni. Katika sehemu ya pili, Mṭhume Muhammad anakuja kwelezewa na Mwalimu Jibril (malaika mtukufu) faida ya hirizi hiyo ambayo ni ya majina maṭukufu ya Mwenyezi Mungu. Mwandishi anatusisitiziya tushikamane na hirizi hiyo ya majina ya Mungu ili itufaidi hapa duniyani na kesho akhera.

Kifani, uṭendi huu unaanza na kumalizikiya kama ṭendi nyengine maarufu za Kiswahili kwa sifa ambazo zimedokezwa na Shariff (1988) na Mazrui na Syambo (1992). Katika utangulizi kuna kumwomba Mungu na kumswaliya Mṭhume Muhammad na jamaa zake. Halafu ni sehemu ya vita baadaye inakuja sehemu ya mafunzo ya hirizi, na hatimaye, kuna kufunga darasa pamoja na maombi kwa waislamu. Mwisho kabisa ni kutaja jina la mṭhunzi na nasaba yake na ṭarehe ya kukamilisha kuṭunga uṭendi huu.

ḌARASA YA SIRI

Tumesema huko nyuma kwamba kufunza Ḍarasani kuna mtinro wake maalumu wa uwasilishaji. Katika mtinro huu kuna miyunro-mbinu ambayo hutumiwa ili lengo linaloṭarajiwa lipatikane. Pili, tumesema kwamba katika kujuwa ṭafauti za lugha/sajili

tunaweza kuangaliya misamiaṭi inayotumiwa pamoja na mitinro ya kusema mawazo hayo. Kwa kufuwata vidokezi hivi viwili, katika sehemu hii tuṭaweka wazi ainaṭi za nrimi alizotḥumiya mṭhunzi wa Siri kwenresha Ḍarasa yake hadi tufunukiwe kwamba Siri ilidhamiriwa kufunza na wala si utambaji wa kihadithi. Kiyelelezo cha Njogu na Chimera (1999, uk. 141) kinaeleza kwamba Ḍarasa, kama inavyopendekezwa na K.I.E (sasa K.I.C.D), ina mpangiliyo huu: Juma (la ngapi katika mfululizo wa ufunzaji), Kipindi, Funzo, Mada, Shabaha (lengo), Somo (hatuwa mbalimbali za somo hilo), Marejeleo, Vifaa, Mazoezi, na Ṭathmini/Kujiṭathmini. Hii nriyo miyunro-mbinu ya mpangilio wa Ḍarasa. Makala haya yaṭachukuwa kiyelelezo hichi kama kurunzi ya kutwangaziya miyunro-mbinu hii lakini hatuṭotumiya mbinu zoṭḥe wakaṭi wa kuuweleza Siri.

Kufungua Ḍarasa

Siri umeanza kama ṭendi nyengine za kale kwa kumtaja Mungu mwanzo kabla ya kuṭhongowa uṭendi wenyewe. Baada ya kumsifu na Mṭhume Muhammad na jamaa zake na kuonesha uṭukufu wa Muumba, Siri unaanza kwa kuṭowa anwani ya uṭendi huu. Mṭhunzi anasema:

21. *Nimependa kunudhumu*
Hadithi ya muungamu
Katiti iliyo tamu
Sikizani watambuzi.

22. *Hadithi hinu hiyari*
Isimu tawakhubiri
Ni Siri li Asrari
Ndio itwao wayuzi.

Katika beṭi hizi mbili mṭhunzi anatḥwambiya jina la uṭendi huu. Katika ubeṭi wa 22 mshororo wa tatu mṭhunzi anasema uṭendi huu waitḥwa *Siri li Asrari* yaani ‘siri ya masiri’. Kimuunro sehemu hii imekuja baada ya sehemu ya utangulizi ambayo ililemeya katika kumuomba Mungu ampe mṭhunzi usahali wa kuṭhongowa uṭendi wake. Kwa hivyo, kwa kutupa sisi anwani ya masimulizi yake, mṭhunzi ametupeleka mpaka Ḍarasani kutwonesha kwamba maneno yake yoṭḥe mada yake ni ‘Siri li Asrari’.

Pili, katika ubeṭi wa 21 mshororo wa kwanza mṭhunzi ametumiya neno ‘nudhumu’ ambalo lina maana ya kiṭaalamu. Hii ni isiṭlahi ya kifasihi

inayotafautisha ‘nudhuma’ na ‘shairi’. Kulingana na Ustadh Mahmoud Mau (maongezi naye Novemba 2012, Lamu) pana tafauti baina ya ‘nudhumu’ na ‘shairi’. Anasema ‘nudhumu’ ni “thungo zenye kumili kwenye mas’ala ya kidini na hasa yaliyothuna na huwa hazina ubunifu (urongo). ‘Shairi’ ni “thungo zenye kulemea kwenye mada ambazo hazina ukali, kama mahaba na mambo mengine ya kikawaida katika jamii.” Thungo za kishairi zaweza kuwa za kibunifu na zaweza kutiwa urongo nrani yake. Tukumbuke neno hili nudhumu ndilo alilothumiya mwenye Al Inkishafi. Kwa hivo, mtunzi alianza utendi wake kwa kutupa anwani ya masimulizi yake na kutwambiya kweupe kwamba ni nudhumu ambayo haina urongo ndani yake. Mas’ala ya kweleza ukweli mtupu (*facts*) hupatikana katika mazingira ya kitaalamu na hukusudiwa kuwapasha habari muhimu wasikilizaji. Lakini piya ni darasani ambako mwalimu hutowa mada ya somo la siku mwanzo wa darasa kama kiyelelezo cha K.I.C.D hapo juu kinavoashiriya.

Usuli Na Kwenreleza Darasa

Kama ilivo katika mapendekezo au tafauti katika tangulizi zao huwa kuna ‘usuli wa tafauti’. Katika sehemu hii huelezwa nrani yake asili ya tasnifu ya mpendekezaji ilianza vipi. Kwa maneno mengine, huweza kwelezwa ilikuwaje mpaka somo hilo la tafauti likaonekana lafaa kutafitiwa. Maelezo haya ya ‘usuli wa somo’ tunayapata katika maelezo ya mukhtasari wa utendi ambao kwetu sisi si hadithi ya vita baina Mthume Muhammad na Andharuni (kutoka ubeji wa 32 hadi 376) bali ni maelezo ya kadimu kuhusu hirizi hii yenye nguvu za kiajabu. Yanateka muhadhara mwanzo kwa kuwapa mapisi ili waelewe maelezo muhimu yatakayokuja baadaye kuhusu hirizi. Kwetu sisi, hii ni mbinu inayopatikana katika sehemu za kitaalamu na maelezo haya yana jukumu yanayotekeleza katika kufikisha tasnifu ya msemaji. Japo twaweza kusema ni utambaji wa hadithi ya kingano kutokana na mathumizi ya lugha ya kitamathali lakini kiufunzaji ina jukumu la kutowa ushahidi wa jambo lililothukiya au kuwapa wanafunzi asili ya watu kufwata au kufanya jambo fulani.

Jinsi ya kupeleka darasa tunaiyona kwanziya ubeji wa 429 – 532. Katika utendi huu, Mwalimu Jibril (mtunzi amemwita hivo nrani ya utendi)

anamweleza kuhusu hirizi ni nini na piya kumpa faida zake. Pili, anamfundisha Mthume Muhammad bila ya yeye Mthume kutiwa neno hata moja katika darasa hii. Tatu, anamfunguliya Mthume Muhammad kwamba hirizi hii ni ya majina matukufu ya Allah. Na mwishowe, anamwambiya kwamba ni jina moja tukufu la Mwenyezi Mungu nriyo liliyomo ndani ya hirizi hino.

Mtinro wa uwasilishaji wa aina hii hupatikana aghalabu katika mihadhara ya kichuwo au makongamanoni. Mhadhiri hupawa nafasi yake aelezee waliyohudhuriya maelezo yake yote bila ya kukatizwa ili mawazo yawaingiye sawasawa waliyohudhuriya. Piya, mhadhiri nriye aliyepawa jukumu la kusema kwa kipinri hicho na wengine wote ni wangoje hadi mwisho ikiwa wana maswali au mushkili wowote waulize. Kwa hivyo, kwa kuwa kuna mhadhiri na kuna waliyohudhuriya taswira hii twaweza kuiyona katika darasa wakati mwalimu anapowafunza wanafunzi kwa sababu yeye nriye mjuzi na wanafunzi wametuliya wakimsikiza mwalimu awambiyayo.

Kurejeleza Mawazo ya Wengine

Kurejeleza mawazo ya wengine yanapotumika katika kazi zozote za kitaalamu nriyo uungwana na inavotakikana kihakika. Mawazo hayo yanapawa marejeleo ili ikihitajika ithibati basi wataalamu watafwatiliya kazi zilizorejelewa na kuhakikisha; kurejeleza mawazo ya wengine ni hatiya kubwa katika taaluma. Mtunzi Mwanalemba hakuwacha kurejeleza hadithi ya utendi huu aliipata wapi. Anasema:

28. *Panenewa, huwambia
Katika hadithi piya
Nyingi zimezotukia
Sahihi ya matongozi.*
29. *Zilio sahihi, tama
Katika hadithi njema
Za mtume wa kadima
Nayo hiyo ni azizi.*
30. *Yalipokewa, yuwani
Na Anasa muumini
Bunu Maliki, mneni
Mola mezompa razi.*

Katika ubeti wa 30 mthunzi anasema maelezo yake yanatokana na upokezi kutoka kwa Anas bin Malik, huyu alikuwa swahaba wa Mthume Muhammad. Katika beti za 28 na 29 mthunzi anat^hwambiya kwamba hii ni Hadithi sahihi – ni ya daraja ya juu katika ukweli. Kwa hivo, anayoyasema mthunzi yana thika ya ukweli na kwamba yanayoelezwa yanafuwata t^harāḡibu za kīṭaaluma ya dini kwa kutaja marejeleo ya mpokezi wa maelezo haya. Mbali ya kutaja mpokezi wa hadithi hii ni nani piya mthunzi anafanya uwaḡilifu wa kīṭaaluma kwa kumtaja shekhe au msimulizi wa kisa hichi kila inapofika haṭuwa ya kuonesha maneno hayo si yake bali ni ya mthu mwengine, shekhe au mpokezi wa hadithi hii. Anaruḡiya usemaji huu mara kadhaa katika Siri, mfano:

108. *Kala Shekhe mtukufu*
Unenee msanifu
Mwenye radhi ya Latifu
Na Mtume muongozi.

148. *Kala shekhe amenena*
Mwenye kurawi maana
Hadithi ya nabiyana
Muhamadi Muhijazi.

Tuṭaona katika beti hizo kwamba mthunzi anat^humiya ‘kala shekhe’ yenye maana ya ‘amesema shekhe’ na ‘amenena mwenye kurawi’ yenye maana ya ‘amesema mwenye kuisimuliya hiyo hadithi’ kurejeleza alivosema huyo mthongowaji wa hadithi. Ni dhahiri kuwa mthunzi mbali ya kuwa ni kazi ya kifasihi lakini alijuwa kaida za kīṭaalamu za kurejeleza mawazo ya wengine ili asije akakoseya adabu za kaida hizo, sembuse kuwafikiyana na mfumo wa uwasilishaji darasani wa Njogu na Chimerah (khj).

Ufafanuzi Juu ya Hirizi

Mwalimu baada ya kuṭowa anwani na kuṭowa kijejezi kuhusu mada anayoiyeleza siku hiyo huweza kuṭowa ufafanuzi zaidi kuhusu mada yake. Kwa mfano, ikiwa mada anayoshughulikiya ina vigawanyo katika maelezo basi aṭaviṭowa hivo vigawanyo ili wanafunzi wapate kuelewa vema mada. Azma ya mwalimu ni wanafunzi waiyelewe dhana pamoja na sehemu kadha wa kadha katika dhana hiyo. Mthunzi Mwanalemba anatupa maana ya hirizi na piya anakuja kut^hwambiya kwamba hirizi hii ina sehemu tatu ndani yake na kila sehemu

ina kazi kubwa inayofanya katika kuṭibu maradhi. Anasema hivi:

455. *Hirizi hinu Mtumi*
Huzidi li aksami
Kwa mara mia msemi
Ifadhiliye wayuzi.

456. *Li aksami shafi'a*
Izidiye manufaa
Kwa ya sefu li kati'a
Ifadhiliye majazi.

457. *Na sefu li kata'ani*
Ifadhiliye yakini
Kwa maratu thalathini
Imezidi maongezi.

458. *Na fadhili yenye siti*
Za sefu li kati'ati
Huzidi mbingu na nti
Kwa mara kumi ndombezi.

Beti hizi zinatupa ufunuwo kwamba hirizi ina ‘aksami’ (ubeti wa 455 mshororo wa pili) yaani ina sehemu/vigawanyo. Kuna sehemu ya ‘kaṭi’a’, ‘kaṭi’aṭi’, ‘kaṭa’ani’ na kila sehemu ina nguvu zake. Sehemu ya ‘kaṭi’a’ (ubeti wa 456 mshororo wa tatu) ina kazi yenye kuleta pozo la magonjwa yoṭ^he. Sehemu ya ‘kaṭi’aṭi’ (ubeti wa 458 mshororo wa pili) ina uwezo zaidi ya uzitho wa mbingu na ardhi mara kumi yake. Sehemu ya ‘kaṭa’ani’ (ubeti wa 457 mshororo wa kwanza) ina nguvu zaidi ya mara thalathini. Nilipomuuliza Uṣṭadh Mahmoud Mau (khj) kuhusu vigawanyo hivi alinambiya yaweza kuwa hirizi hii ni hiyo hiyo moja lakini mthunzi ameipa sehemu kadhaa kwa sababu ya kuṭimiza arudhi ya kina katika uṭ^hendi. Walakini, kwa dhahiri na maelezo ya mthunzi mwenyewe katika uṭ^hendi, tunaona kwamba kuna sehemu tatu za hirizi hii ṭukufu na kila moja ina kazi na uwezo wake. Kidarasa huu ni ufafanuzi wa ziyada ili wanafunzi waelewe kwa uzuri dhana ya hirizi na vigawanyo vake.

Faida za Hirizi

Katika masomo ya, kwa mfano, jiografiya ya binadamu, wanafunzi huelezwa sekta zoṭ^he za kiuchumi nchini na piya huelezwa faida za sekta mbalimbali zinavojenga nchi. Mbinu hii ina ushawishi wa kuwaṭaka wanafunzi watiliye maanani sekta hizi na wao wajishughulische katika

ujenzi wa taifa kupitiya sekta hizi. Mfano huu wa kutowa dhana na halafu kutowa faida iliyo nazo kwa binadamu tunaushuhudiya katika Siri. Katika utendi huu mthunzi ametowa faida kumi na sita za hirizi na

ameziratibisha moja baada ya nyengine katika beti moja moja kama wafanyavo walimu wa shule madarasani. Kuhusu faida ya hirizi mthunzi anat^hwambiy:

402. *Ni matukufu pulika
Maina yakwe Rabuka
Na mtu mwenye kwandika
Menali mangi majazi.*

404. *Mtu hoyo m^{fa}dhala
Kinwa maina ya Mola
Wepukane na madhila
Milele hana kinyezi.*

405. *Hangiwi maisha yake
Ni msiba mpulike
Katika moyoni mwake
Ila kwitwa ni Azizi.*

406. *Walau hamu na ghamu
Hawi nayo kwa dawamu
Mtu hoyo muadhamu
Mungu amemhifazi.*

407. *Na siku hiyo bashiri
Ya Kiyama kudhihiri
Hufungamana umuri
Na maina ya Muyuzi.*

472. *Dua hinu Mustwafa
Ni kama mtu wa sifa
Alowakifu Arafa
Siku ya Juma muyuzi.*

473. *Thawabuze tatongowa
Mtu takoitukuwa
Dua hinu ya sitawa
Hapati la kumuuzi.*

474. *Siku ya kufa basiri
Hawaonani umuri
Na Munkar wa Nakiri
Hawamwandiki maozi.*

475. *Wala kabisa haoni
Zituko za kaburini
Mtu hoyo kwa yakini
Ya Rabi memhifazi.*

476. *Yuwa mtume rasuwa
Dua hinu ikuziwa
Ulimwenguni ni dawa
Kwa kula mawi marazi.*

477. *Na Ahira ni zaidi
Hutekeleza ahadi
Na kuokoka na abadi
Na harufu na kinyezi.*

479. *Humpa Mola Mkwasi
Pepo ya Firdausi
Kangiya ndani upesi
Ziunguni kabarizi.*

507. *Manufaaye basiri
Nda Rihi li Ahmari
Huziwiya kula shari
Na baa za wazimzi.*

516. *Na yambo ulitakalo
Lolote ulipendalo
Ukalinuwiliyalo
Hulipata uli razi.*

Katika beti hizo hapo juu, maneno tuliyoweka kwa herufi za mlazo nrizo faida za hirizi. Tunafahamishwa kwamba hirizi hii inaweza kujibu: magonjwa ya kiwiliwili (ubeti wa 404, 405, 406), magonjwa ya kiakili ya majini wabaya (ubeti wa 507), kuepusha mateso ya kaburini (ubeti wa 474, 475), mwenye hirizi hii haogopi misukosuko ya siku ya kiyama (ubeti wa 407, 477), na huko akhera mthu huyo atapawa pepo ya juu kabisa ‘janna^{tu} firdausi’ (ubeti wa 479). Niya ya mthunzi-mwalimu ni kutaka kushawishi kwamba hirizi hii inaweza kufanya kazi

bila wasiwasi tena anatuonesha mahali na wakati gani.

Hitimisho La Darasa

Wakati mwalimu anapokaribiya kufunga darasa yake huweka sehemu ya hitimisho ili kutowa mukhtasari na piya kusisitiza lengo la somo hilo. Hii ni mbinu ya kimasomo ili kusakinisha mawazo ambayo yameolewa katika darasa na kumshawishi msikilizaji akubali yale aliyoelezewa baada ya kuyafahamu. Bakhtin anasema katika masamezano

huwa kuna 'sentensi za mstari wa mbele' ambazo, mosi, hujulisha mipaka ya kauli za wasemezanao na, pili, hubeba msisitizo wa yale yaliyosemwa katika kauli nzima. Ni mpaka kwa sababu huonesha kauli ya mthu mmoja iliyanza wapi na imekomeya wapi. Sentensi hizi huwa na sifa ya kurudiliya niya yenyewe ya maneno kusemwa. Katika u^gendi huu kuna be^{ti} mbili ambazo ziko mbali mbali kimaweko lakini zasema kauli moja. Mthunzi anasema hivi:

*Tena ina manufaa
Mtu atakaovaa
Humwepukiya baa
Na zitimbi za gharazi.*

551. *Hirizi hinu wendaka
Mtu kombe kilandika
Anwapo na kuipaka
Hasaliwi ni marazi.*

Be^{ti} hizi mbili ambazo ziko mahala ^{ta}fauti katika u^gendi zinarejeleza jambo moja – umuhimu wa hirizi hii ya majina ya Mwenyezi Mungu. Katika ube^{ti} wa 25 mthunzi anat^hwambiya kwamba hirizi hii mthu atakapokuwa nayo basi hashikwi na magonjwa yoyot^he. Na katika ube^{ti} wa 551 mthunzi anaregeleza mawazo yayo hayo. Mwanzo wa u^gendi anatupa fununu kwamba hirizi hii ina manufaa makubwa na katika hitimisho lake la u^gendi piya anat^hwambiya vivyo. Juu ya kwamba ni sentensi za mstari wa mbele lakini kwetu sisi be^{ti} hizi zaonesha hitimisho la mwalimu katika ^{da}rasa yake na zasisitiza kauli yake tangu mwanzo kwamba maelezo anayoyag^owa nriyo 'siri ya masiri'.

HITIMISHO

Makala haya yamejaribu kupinruwa kauli kwamba ^gendi za kabla ya karne ya ishirini zilitungwa kweleza mapisi ya mthu/jamii ^{tu}. Kutokana na miyunro-mbinu ya namna mthunzi anavoenreleza maudhui yake imedhihirika kwamba Mwanalemba alikuwa na dhamira ya kutufunza kuhusu hirizi na umuhimu wake na aligawanya ^{da}rasa yake katika vigawanyo venye kulanrana sawasawa na maelezo ya K.I.C.D. Hatukuchukuwa kiyeelezo chote cha K.I.C.D kuwa mfano wa kuenresha ^{da}rasa ya mthunzi bali tumetaka kuonesha, kwa ithiba^{ti}, kwamba kufunza kuna muunro unaopendekezwa na ^{ta}asisi za kielimu. Kwa kufwata muunro huu, tumedhihirisha madhumuni mbalimbali

aliyot^humiya mthunzi wa Siri ili kutufunza ^{da}rasa yake juu ya hirizi: vigawanyo vake, ufaafu wake kwa magonjwa tuyaona na tusiyoyaona, na ithiba^{ti} ya kufanya kazi kwake katika hali ya kijamii kama kwenye vita baina ya Mthume Muhammad na Andharuni. Kutokana na tuliyobainisha ni wazi Mwanalemba alitupa ^{da}rasa na alilipanga namna ya kutu^guza mengi katika ^{da}rasa hiyo na kwamba si kama inavofikiriwa kwamba ^gendi za Kiswahili za kabla ya karne ya ishirini ni utambaji wa hadithi za kingano tu. T^hwaregeleza tena kuwa u^gendi wa Siri bado haujashughulikiwa kwa mapana na marefu yake kuna mas'ala yasiyo ya kidini kama muktadha na mandhari ya kutungwa kwake yahitaji ufafanuzi ili upate kweleweka kwa uzuri zaidi.

MAREJELEO

- Bakhtin, M. M. (1981). *The dialogic imagination*. Micheal H. (mtafsiri na mhariri) Austin: The University of Texas Press.
- Bakhtin, M.M. (1986). *Speech genres and other late essays*. Caryl, E. & Micheal H., (wah.) Austin: The University of Texas Press.
- Chimerah, R. M. (1989). *The implications of the selected works of Ngugi in the educational thinking and practices of Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijchapishwa). Ohio University, Ohio.
- Dammann, P. E. (1940). *Dichtungen in der Lamu mundart des Suaheli* Band 28. Hamburg: Freiderichsen.
- Mazrui, A. & Syambo, B. K. (1992). *Uchambuzi wa fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Shariff, I. N. (1984). Letters to the Editor. *Katika Research in African Literatures*, 15 (1), 150-156. Imesomwa <https://www.jstor.org/stable/3819755>.
- Shariff, I. N. (1988). *Tungo zetu: Msingi wa mashairi na tungo nyenginezo*. New Jersey: The Red Sea Press.